Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

15th Shawwal 1431
24th September, 2010

Volume 2, Issue 4

Hadeeth Ya "Ghoul"

Mtayarishi: Sheikh Mash-hur Hassan Salmaan

Abu Hurairah (رضي الله عنه) amesimulia:

"Mtume (صلى الله عليه وسلم) alinihaliwisha kulinda *Zakaah* za *Ramadhaan*. Akaja mtu mmoja na kujaribu kuchukuwa baadhi ya chakula, mimi nikamshika na nikasema, 'Wallaahi! Nitakupeleka mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) Akasema, 'Mimi ni masikini, nina jamii (wenye kunitegemea), na niko kwenye hali mbaya ya mahitaji!" Kisha nikamuacha ende zake.

Ilipofika asubuhi, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaniambia, *"Ewe Abu Hurairah! Mfungwa wako alifanya nini jana?"* Nikasema, 'Ewe Mjumbe wa Allaah! Alilalamika yakwamba yeye alikuwa ni masikini, na kwamba alikuwa na jamii (ya kuiangalia), na kwamba alikuwa kwenye hali mbaya ya mahitaji. Kwahivyo, nikamuhurumia na nikamuacha .' Akasema (Mtume (صلى الله عليه وسلم), *"Lakini alikudanganya na atakuja tena."*

Kwa vile Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliniambia hivyo, nilijua yakwamba atakuja tena kwahivyo nilimungojea. Alipoanza kuchukuwa chakula nikamshika na nikamwambia, 'Nakuchukuwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) Akasema, 'Niwache, kwani mimi ni masikini na nina jamii (ya kuiangalia). Sitorudi tena.' Kwahivyo, nikamuhurumia na nikamuacha.

Asubuhi, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaniambia, *"Ewe Abu Hurairah, alifanyaje mfungwa wako?"* Nikasema, Ewe Mjumbe wa Allaah! Alinilalamikia yakwamba alikuwa ni masikini, na alikuwa na jamii (inayomtegemea), na kwamba alikuwa kwenye hali mbaya ya mahitaji!'. Kwahivyo, nikamuhurumia na nikamuacha ende zake .' Akasema (Mtume (صلى الله عليه وسلم) *"Lakini alikudanganya na atakuja tena."* Basi nikamungojea kwa mara ya tatu.

Alipoanza kuchukuwa chakula, nilimshika na nikamwambia, 'Nitakupeleka mpaka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Hii ni mara ya tatu! Na uliniahidi yakwamba hutorudi tena, lakini hivyohivyo ukarudi!' Akaniambia, 'Niwache niende zangu, nitakufundisha maneno ambayo Allaah atakufaidisha nayo.' Nikamuuliza, 'Ni maneno gani hayo?' Akajibu, 'Kila uwendapo kulala, soma Aayat al-Kursee – *Allaahu laa ilaaha illaa huwa al-hayyu al-qayyum* - mpaka mwisho wa Aya hiyo. Kisha Allaah atakuwekea mlinzi abakie na wewe, na wala hutokurubiwa na Shaytaan yoyote mpaka asubuhi.' Basi nikamuacha ende na njia yake.

Kisha asubuhi, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaniambia, *"Jana mfungwa wako alifanya nini?"* Nikamjibu, 'Ewe Mjumbe wa Allaah! Alidai yakwamba atanifundisha mimi maneno ambayo Allaah atanifaidisha nayo. Basi na mimi nikamuacha ende zake.' Akasema (Mtume (صلى الله عليه وسلم) *"Na ni mameno gani hayo?"* Nikamwambia, 'Alisema, "Wendapo kulala isome Aayat al-Qursiyy' kuanzia mwanzo mpaka mwisho, *Allaahu laa ilaaha illaa huwa al-hayyu al-qayyum*. Kisha Allaah atuwekea mlinzi abakie na wewe, na wala hutokurubiwa na Shaytaan yoyote mpaka asubuhi."

Mmojawapo wa wapokezi akaongezea, "Na wao (maswahaba) walikuwa daima wakitafuta mambo mazuri." Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema, *"Alikwambia maneno ya kweli, lakini yeye ni mrongo. Unamjua uliyezungumza nae kwa hizo siku (nyusiku) tatu, ewe Abu Hurairah?"* Akajibu Abu Hurairah, "Laa." (Mtume (صلى الله عليه وسلم) Akamwambia, *"Huyo alikuwa ni Shaytaan."*

Hadeeth hii ni maarufu sana iliyopokewa na al-Bukhaari kwa njia ya *mu'allaq* katika swaheeh yake, na vilevile *at-Taareekh ul-Kabeer*. Masimulizi yake pia yamedondolewa na al-Baghawee. Na ziyada, Ibn Hajar ameonyesha yakwamba msururu wa wapokezi wa hadeeth hiyo umeunganishwa kwa njia nyingi.

Katika *Fat-hul-Baari*, Ibn Hajar ametaja mambo mengi ambayo tunaweza kujifunza kutokana na hadeeth hii, mbali na baadhi ya fadhla za *Aayat ul-Kursee*, hapa chini ni baadhi yake:

* Yakwamba *Shayateen* wanayaelewa mambo yenye kumfaidisha *mu'min*.
* Yakwamba Hikma inaweza kupatikana kutoka kwa mtu muovu. Na, ingawaje mtu muovu hakufaidika na hikma hiyo, wengine huwenda wakafaidika nayo.

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 2)

Yaliyomo

Hadeeth ya "Ghoul" 1 - 4

Zinyoe Zote au Ziwache ... 4

HADEETH YA "GHOUL"

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

* Yakwamba mtu anaweza kujua jambo fulani na asiweze kulitendea kazi.
* Yakwamba *kaafir* anaweza kuyaamini baadhi ya anayoyaamini *mu'min*, lakini hayo yasiweze kufanya yeye awe ni *mu'min*.
* Yakwamba mrongo anaweza kusema ukweli.
* Yakwamba kwa kawaida *shayateen* ni warongo.
* Yakwamba wanaweza kujitokeza kwa njia ya kuonekana na sisi, na kwamba hiyo Aaya (kama ilivyofasiriwa) hapo chini, ni makhsusi inayowahusu *shayateen* pindi wanapokuwa kwenye umbile lao la asili.**"... hapana shaka yeye (shetani) na jeshi lake yuwawaona kwa namna musiyowaona."** [al-A'raaf 7:27]
* Yakwamba *Jinn* hula chakula cha wana-adamu.
* Yakwamba wanaweza kujitokeza kwa wana-adamu, kwa njia isiyokuwa hiyo iliyotajwa hapo juu.
* Yakwamba wanaweza kuzungumza lugha za wana-adamu.
* Yakwamba wao ni wevi na walaghai.
* Yakwamba *Jinn* anakula katika chakula ambacho hakikutajwa jina la Allaah juu yake.
* Yakwamba mkono wa mwivi haukatwi kwenye hali ya ukame.
* Kukubali udhuru wa mtu na kumsamehe uanpodhania yakwamba anasema ukweli.
* Inathibitisha utambuzi wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika mas'ala yaliyofichika.
* Kuruhusiwa kupokea Zakaat-ul-Fitr katika usiku wa kabla ya fitr, na kumuwakilisha mtu kuilinda.

Kuna ahaadeeth nyingi kama hiyo ya Abu Hurairah, zenye kutaja fadhla za *Aayat-ul-Kursee* na mgeni wa kushangaza aliyejitolea kumueleza swahaba kuihusu. Ufuatao ni mfano, na sasa jina la mgeni ni Ghoul:

'Abdur-Rahmaan bin Abu Laylaa amepokea, "Siku moja ghoul (sheytaan wa kike) alikuja kwenye ghala la Abu Ayyub na akamshika. Akenda kumshtakia Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusu tukio hilo, nae akasema, *"Utakapomuona, basi sema, 'Kwa Jina la Allaah, njoo na umuitikie Mjumbe wa Allaah."* Basi akarudi tena , naye akamwambia hayo aliyoambiwa na akamshika; kisha akamwambia, 'Sitorudi tena.' Basi akamuacha. Akarudi tena na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia, *"Alifanyaje mfungwa wako?"* Akasema, "Nilimshika, lakini akasema hatorudi tena. Kwahivyo, nikamuacha ende zake." Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم) *"Atarudi tena.*

Nimemshika mara ya pili na mara ya tatu; na kila mara yuasema hatorudi tena. Basi mimi nikenda kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akaniuliza, *"Mfungwa wako alifanyaje?"* Akasema, "Nilimshika, lakini alisema yakwamba hatorudi." Mtume (صلى الله عليه وسلم)akasema, *"Atarudi."* Basi akamshika tena, na akasema, "Niwache na nitakufundisha kitu ukiseme; na hakuna chochote kitakachokukurubia. Ni Aayat-ul-kursee. Basi akaja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamueleza. Akasema, *"Amekwambia ya kweli, na yeye ni mrongo."*

Hadeeth hii imepokewa na Ahmad, at-Tirmidhee na wengineo

'Abdullaah bin Ubayy amesimulia yakwamba babake alikuwa na ghala la kuhifadhia tende. Aliingia ndani (ya hilo ghala) siku moja akagundua yakwamba baadhi ya tende zimekosekana. Kwahivyo akashika zamu hapo. Mara akamkuta ndani, mnyama aliyefanana na kijana barobaro. Akasema, "Basi nikampa salaam, naye akanirudishia salaam", nikamuuliza, "Wewe ni nani, ni Jini au mwana-adamu?" Akanijibu, "Ni Jini", nikamwambia, "Hebu nionyeshe mkono wako". Akanionyesha mkono wake; ulikuwa ni mkono wa Jibwa uliokuwa na nywele kama za Jibwa. Nikamwambia, "Hivi ndivyo Majini walivyo? Akanijibu, "Mimi nawajua Majini walio wabaya kuliko nilivyo mimi." Ubayy akamwambia, "Ni lipi lililosababisha mpaka ukafanya uliyoyafanya?" Akamjibu, "Sisi tumejua yakwamba wewe ni mtu upendaye kutoa swadaka, kwahivyo, tumependelea kupata baadhi ya chakula chako." Ubayy akasema, "Kuna jambo lolote liwezalo kutulida sisi na nyinyi?" Akasema, "Aya hii: Aayat-ul-qursee. [yoyote atakaeisoma wakati wa jioni atalindwa kutokamana na sisi mpaka usiku.]" Siku iliyofuata, Ubayy alikwenda kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akampasha habari kuhusu yaliyotokea. Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم) *"Muovu amesema kweli."*

Hadeeth hii imepokewa na an-Nasaa'ee katika *'Amal al-Yawm wal-Laylah*, al-Baghawee katika *Sharh as-Sunnah,* al-Bukhaari katika *at-Taareekh al-Kabeer,* Ibn Hibbaan katika *Swaheeh* yake, na wengineo.

Kuna hadeeth nyengine kama hii, kwa daraja zinazotafautiana za uswaheeh, na kwenye riwaya nyengine wapokezi wamemwita kiumbe huyo ghoul; mara nyengine kiumbe huyo alikuwa ni mume, na mara nyengine alikuwa ni mke. Miongoni mwa riwaya nyengine zenye kufanana na hii ni riwaya ya Mu'aadh, Buraydah, na Abu Usayd, wawili wao wa mwisho ambao waliomtaja ghoul. Hadeeth zote hizi zinaunga mkono kuwepo kwa ghoul kutokana na mapokezi yao mengi. Huu ndiwo msemo wa Ibn Hajar katika *Fat-hul-Baaree*, al-Baihaqee katika *Dalaa'il an-Nubuwwah,* Ibn Katheer kwenye *Tafseer* yake, na al-Mubaarakpooree katika *Tuhfat al-Ahwathee*. Baada ya riwaya ya Abu Ayyub, al-Haakim

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

HADEETH YA "GHOUL"

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

akasema, "Silsila hizi za riwaya, zikiwekwa pamoja, zinaifanya daraja ya hadeeth kuwa *Mash-hoor* (iliyo mashuhuri), na Allaah Ndiye Mjuzi Zaidi."

Ghoul ni Kitu gani?

Jina maarufu la Majini waovu litakuwa ni *Shayaateen*, na ghoul anaingia kwenye orodha hii. Hatahivyo, rai chungu nzima zimetaja hali halisi na maumbile ya ghoul. Baadhi yao zimefikilia kudai yakwamba ghoul ni aina ya tumbiri!

Amma kuhusu neno lenyewe "ghoul" (wingi: *ghilaan*), limetokana na mojawapo ya maana ya neno lenye kumaanisha kuuwa (bila ya sababu) au kuuwa (kwa sababu za kisiasa au dini); *ightigaal* kwa mfano. Kamusi maarufu za kiarabu zimefasiri ghoul kuwa ni mchawi au mganga miongoni mwa Majini. Baadhi ya watu wamesema yakwamba ghoul ni neno litumuwalo kwa Majini wenye kuonekana nyakati za usiku, na kwamba si'laah ni neno litumiwalo kwa Majini waonekanao nyakati za Mchana. Katika tafsiri yake, Ibn Katheer amesema yakwamba ghoul hutumiwa kwa Majini wakitokeya nyakati za usiku. Amesema Al-Jaahiz, "Ni jina la kila Jini ambaye msafiri hupambana nae, anayejitokeza kwa sampuli na umbile tafauti, mke na mume. Ibn Hajar ameidhinisha Rai yakwamba ghoul anaweza kubadilisha umbile lake kutokana na uchawi. Rai hii imeungwa mkono na hadeeth ya Ubayy hapo juu, hadeeth ya Mu'aadh na vilevile riwaya kutoka kwa Abu Ayyub inayomtaja ghoul mwanzo akijitokeza kama paka, na kisha akibadilika. La zaidi ni kwamba rai hii imeungwa mkono na taarifa iliyonukuliwa na 'Abdur-Razzaak katika *Musannaf* yake yakwamba 'Umar (رضي الله عنه) alisifiwa jinsi ghoul alivyo na akasema, "Hakuna kiwezacho kumbadilisha katika umbile aliloumbiwa isipokuwa kwa njia ya uchawi, kwahivyo *waadhinie* unapowaona wakifanya hivyo."

Taarifa Zenye Kumkanusha Ghoul

Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Hakuna 'adwaa, hakuna tiyarah, na hakuna ghoul*." [Muslim]. Kuna ahaadeeth nyingi kama hii zenye kutaja taarifa, '*Laa (hakuna) ghoul*'. Zinapatikana kama hizo katika al-Bukhaari na Muslim na pia wengineo. Kwa kuzingatia mjadala uliotangulia wenye kuthibitisha mas'ala ya ghoul, ufuatao ni ufafanuzi wa wanavyuoni wenye kurekebisha ikhtilafu inayodhihirika baina ya *Nass* mbili. Taarifa isemayo "Hakuna ghoul" haikatai kuwepo kihakika kwa ghoul, lakini inakataa ushirikina uliokuwa ukitekelezwa katika zama za *Jahiliyyah* kuhusu ghoul. Yaani, yakwamba wao ndiwo wenye kuuwa, yakwamba wao ndiwo wenye kuwateka nyara wasafiri kutoka kwenye barabara, na kwamba wao wanakula watu. La ziyada, Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema '*Laa (hakuna) ghoul',* alisema kama hivyo pia kuhusu mambo mengine, kama '*adwaa* kwa mfano. Na bado akaamrisha kuhusu aina fulani ya '*adwaa* katika matukio mengine, kama vile kukimbia kutoka katika sehemu iliyoathiriwa na ugonjwa wa tauni utakapoarifiwa kuhusiana nao kabla hujafika mahali hapo. Na katika mabadiliko ya hadeeth moja yenye kutaja '*adwaa*, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "*Lakini mkimbieni mkoma (mwenye ugonjwa wa ukoma) kama mutakavyomkimbia Simba*." Haya yote ni yenye kuhusiana na Qadar ya Allaah. Yaani, waumini hawafai kuamini yakwamba kuyakimbia maradhi ndiyo njia ya pekee ya mtu kujiokoa nayo. Hii ndiyo tafsiri ya wanavyuoni kama al-Baihaqee, Ibn as-Salaah, Ibn Rajab, na wengineo. Kwahivyo, Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakukanusha kuwepo kwa '*adwaa*, alichokanusha yeye ni kule kuiamini kwao kabla ya uislamu. Ibn Jareer at-Twabaree amesema, "Kwa kusema kwake Mtume (صلى الله عليه وسلم), "*Laa ghoul",* alikuwa akikanusha yale yaliyokuwa yakisemwa na watu katika zama za Jahiliyyah kuihusu. Yaani, kuhusu uwezo wake wa kudhuru, kunufaisha, na kuwapeleka watu kwenye njia hiyo... na hii ni sawa na yaliyobaki katika aliyowahi kuyataja yakwamba Waarabu waliamini yatamdhuru au yatamnufaisha, kama '*adwaa, safr, na tiyarah* (ishara mbaya). Amesema Imaam an-Nawawee, "... na maana ya '*Laa ghoul',* ni kwamba hawana uwezo wa kumpotoa yoyote...."

Silaha Za Kupambana Na Ghoul

Yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo yaliyotajwa na wanavyuoni ya kuweza kuwafukuza ghoul:

Kulitaja Jina la Allaah

Hili limetajwa kwenye hadeeth ya Abu Ayyub hapo awali.

Kusoma Aayat al-Kursee

Katika hadeeth zilizotangulia, hawa ghoul wenyewe wametufahamisha yakwamba jambo hili litatulinda dhidi yao, na akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba hayo yalikuwa ni ya kweli.

Kukaa ndani wakati wa usiku wa manane

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم) **:**

"Jitahadharini na kukutana baada ya usiku unapotanda, kwani huwa hamujui ni viumbe gani ambavyo Allaah huviachilia (kuzunguka wakati huo)." [al-Haakim, imepewa daraja ya Hasan na al-Albaani katika as-Swaheehah 4:346].

Muadhini

Wanavyuoni wameafikiana yakwamba

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

HADEETH YA "GHOUL"

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

shayaateen huondoka pindi muadhini unapoadhiniwa. Kuna ahaadeeth nyingi zenye kueleza hayo, na baadhi zake zinaeleza kuhusu kuadhini wanapotokeza ghoul. Kuhusiana na uswaheeh wa hadeeth, msimamo huu umeungwa mkono na muungano wa hadeeth zenye kumtaja ghoul. Hususan inapochukuliwa na taarifa iliyo swaheeh kutoka kwa 'Umar (رضي الله عنه) iliyowahi kutajwa hapo awali, ambayo daraja yake ni *hukm marfu'* – au hukmu iliyoinuliwa mpaka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم)

Kwa kumalizia: Hatimae, mafunzo muhimu zaidi kutokana na riwaya za ghoul, ni kwamba huwenda ikawa mtu anaijua sehemu ya Qur'aan – hata huwenda akafika daraja ya kuwa ameihifadhi Qur'aan nzima – na hata kama huwenda akawa na 'ilmu kiasi kikubwa kuhusiana na fadhla zake na faida nyenginezo kuhusiana na Dini, hiyo haimaanishi yakwamba kila kitu asemacho kina thamani kukisikiliza.

Zinyoe Zote Au Ziwache Zote Zikuwe!

Katika hadeeth iliyo swaheeh iliyopokewa na Abu Daawud, an-Nasaa'ee, na wengineo, Ibn 'Umar (رضي الله عنه) amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimuona kijana aliyekuwa amenyoa sehemu ya kichwa chake na kuiwacha sehemu nyengine. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawakataza (maswahaba) kufanya hivyo, akasema: «*Zinyoe zote au Ziwache zote zikuwe*»".Al-Bukhaari, Muslim na wengineo pia wamepokea hadeeth inayohusiana nayo, ambamo Ibn 'Umar (رضي الله عنه) amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliharamisha *al-qaza'a'*."

Ufafanuzi

Aliulizwa Naafi', "Ni nini *al-qaza'a'*?" Akasema, "Ni pale kijana anaponyoa sehemu ya kichwa chake na kuiwacha sehemu nyengine." Katika riwaya iliyopokewa na al-Bukhaari, alisema, "Ni pale kijana anaponyoa na kuwacha (nywele) hapa, hapa, na hapa. 'Ubaydullaah bin Hafs, mpokezi kutoka kwa Naafi', kisha akaashiriya kwenye sehemu iliyo mbele na sehemu za pande mbili za kichwa chake. 'Umar bin Naafi', aliyeipokea hadeeth hiyo kutoka kwa Naafi', akaendelea kuifafanua: "Inaruhusiwa kunyoa nywele kwenye panja (komo) la kichwa cha kijana au kuziwacha nywele kwenye kishogo. *Al-qaza'a'* ni kuziwacha nywele sehemu ya mbele ya kichwa peke yake na kuzinyoa sehemu nyengine, ili kichwa kionekane kama kwamba kimegawanywa sehemu mbalimbali ..." Ibn Abee Shaybah amepokea kama hivyo kutoka kwa Ibraahim an-Nakha'ee. Imaam an-Nawawee akauidhinisha ufafanuzi wa Naafi'. Akaongezea yakwamba udhuru unaweza kupatikana kwa lengo la kutibu maradhi. Ibn Hajar akaelezea: "Baadhi ya wanavyuoni wameshikilia rai yakwamba *al-qaza'a'* imeharamishwa kwa sababu inaharibu umbile la mtu, wengine wanasema yakwamba ni sura za shaytaan, na wengine yakwamba ni sura za Mayahudi... *Al-qaza'a'* ni kwenye mipaka ya nywele za kichwani, sio nywele za sharafa au za kishogo."

Utekelezaji

Maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) «*Zinyoe zote au Ziwache zote zikuwe*», yananukuliwa sana kwenye zama zetu kama dalili ya kuwaharamisha wanaume kunyoa nywele zao kwa mtindo unaosababisha baadhi ya sehemu kuwa ni fupi kuliko nyengine. Kutokana na ufafanuzi wa hapo juu wa watu wema waliotutangulia ni dhahiri yakwamba hivyo sivyo, mpaka sehemu za nywele kwenye kichwa zinyolewe kabisa kama wanavyofanya mohawk au kama ilivyo kawaida siku hizi ambapo sehemu moja au zaidi hunyolewa kabisa. Hatahivyo, jambo hili lisimuhimize yoyote aige mitindo ya nywele inayofanana na wasiokuwa-Waislamu. Kama alivyofafanua Ibn Hajar hapo juu, baadhi ya wapokezi wamesema kuwa sababu ya kukatazwa ni kufanana kwake na Mayahudi. Kama hukmu ya ujumla, kila mtindo wa nywele ukizidi kufanana na wasiokuwa-Waislamu, kuharamishwa huzidi kutokana tu na makatazo ya ujumla wa kufanana na wasiokuwa-

P. O. Box 85477,
Mombasa,
Kenya.

E-mail: info@qssea.net

QSS (E.A)

جمعية القرآن والسنة في شرق إفريقيا

Tuko katika Tovuti

http://www.qssea.net